

Ukweli Hauna Kutu

Pambazuko

Toleo Namba 019

Jumatatu Novemba 14-20

**Majaliwa shujaa,
nani awajibike?
Uk. 5**

**PSSSF yalamba
faida bilioni 582/-
Uk. 7**



Hasira za Samia kuonekana leo

Mawaziri matumbo joto

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

Walipwe fidia haraka

INATARAJIWA kwamba Novemba 20, mwaka lhuu – wiki moja kuanzia leo, matokeo ya awali ya uchunguzi wa kitaalamu kuhusu chanzo cha ajali ya ndege ya Kampuni ya Precision Air, yatawekwa hadharani, hivyo kutoa fursa kwa masuala mengine kuendelea ikiwamo mchakato wa kulipwa fidia kwa waliopoteza maisha na walioumia.


Ajali ya ndege hiyo ilitokea baada ya kutumbukia Ziwa Victoria, nje kidogo ya Uwanja wa Ndege wa Bukoba, Kagera ambapo watu 19 walifariki dunia.

Pamoja na kuendelea kuwapa pole wafiwa na kuwatakia uponaji wa haraka manusura, Pambazuko linahimiza kuharakishwa kwa mchakato wa kulipa fidia kwa watu wote waliohusika katika ajali hiyo.

Tunahimiza watu hao kulipwa haraka fidia zao kwa kuwa kuendelea kuwachelewesha stahiki zao, ni kuongeza mzigo mwingine wa “machungu” kwa familia na wahusika walionusurika.

Uzoefu wa kulipa fidia kwa kampuni nyingi baada ya kutokea kwa ajali hapa nchini unaonyesha kwamba huchukua muda mrefu mno.

Ni vyema basi, serikali kama ambavyo imeeleza tangu awali kwamba itasimamia taratibu zote za mazishi, basi iendelee na kusimamia suala la kulipwa kwa stahiki kwa familia za waliopoteza maisha na hata wale walioumia katika ajali hiyo.



Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: pambazuko1@protonmail.com ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



*KILA siku tunahitaji kufanya vizuri zaidi, lakini kufanya vizuri zaidi kesho kuliko jana na juzi, iwe msingi wa kuondokana na ufukara wa kile tunachokifanya kwa ajili ya maisha na nchi yetu – **Reginald Mengi**. Mengi ambaye sasa ni marehemu alikuwa mmoja wa mambilionea wakubwa Tanzania.*

Ni salama zaidi kuishi kama waliokuwamo Precision Air

Na Askofu Severine NIWEMUGIZI

NDEGE ya kampuni ya usafiri wa hanga ya Precision Air, ilitua kwa dharura ndani ya maji ya Ziwa Victoria, mita chache kabla ya kuufikia uwanja wa ndege wa Bukoba, mkoani Kagera. Hii ilikuwa Novemba 6, 2022 majira ya asubuhi.

Kutua huko kulikuwa ni ajali ambayo ilisababisha vifo vya watu 19, huku wengine 24 wakiokolewa na wavuvi na baadhi ya wafanyakazi wa kiwanja hicho cha ndege.

Mengi yameendelea kuzungumzwa kuhusu chanzo cha ajali hiyo; wapo wanaohoji sababu hasa za rubani kuamua kutua ndani ya maji kwa dharura, kwanini hakuamua kurejea Mwanza kama hali ya hewa haikuruhusu, je, waliokuwa wakimuongoza hakuwasikiliza, je, walimshauri nini?

Hakika maswali ni mengi sana na hayana majibu sahihi kwa sasa kwa kuwa mhusika wa kuyajibu haya hayupo duniani. Alikuwa miongoni mwa watu hao walipoteza maisha yao kwenye ajali hiyo.

Itoshe tu sasa kusema kwamba – “walale mahali panapowastahili na tumuombe Muumba wetu awasamehewe makosa yao.”

Hata hivyo, wakati tukiendelea kuomboleza ndugu zetu hawa, ni muhimu kutafakari mengi juu ya yale yaliyotokea na hasa hali za abiria na wafanyakazi waliokuwamo ndani ya ndege hiyo iliyobeba abiria 43.

Ileweke kuwa mawazo ya waliokuwamo ndani ya ndege kabla ya uokozi ni mawazo ya kipekee.

Hawa hawakuwaza benki wana shilingi ngapi, hawakuwazi simu ya macho matatu, hawakuwazi majumba wala kuwa na magari ya kifahari.

Hawakuwaza “kula bata,” hapo walipokuwepo waliwaza tu “sala zao za mwisho.”

Hawakuwazi kwamba wana shahada



zangu tatu (PhD), hakuna aliyewaza kwamba sasa shahada zake mbili (masters) zinapotea bure na kwamba alipoteza muda na pesa zake kusoma.

Uhakika ni kwamba wote waliwaza namna maisha yao sasa yanakwenda kuhitimishwa kwenye ajali ya ndege ambayo waliamini itawafikisha salama Bukoba.

Hawa wangeambiwa kwamba kupona kwao kunahitaji Sh. milioni 10, hakika kila mmoja angetoa kwa njia yoyote ile; iwe kwa kukopa, kuchukua akiba yake, kwa kuuza mali alizonazo na vyanzo vingine, ilimuradi apone.

Hawa wangeambiwa wakane vyti vyao vya kuhitimu elimu zao, wakatae nafasi walizonazo kwenye ajira zao au hata kugomea uhusiano wao, wangekubali ili tu wanusurike.

Hali walizokuwa nazo watu hawa kabla ya kuokolewa zinadhiri kwamba uhai wa binadamu ni muhimu zaidi kuliko kitu chochote kile.

Hivyo, ni vyema kujifunza kwamba haya maisha tunapaswa kuishi kama tupo ndani ya ndege ambayo ilipata ajali, kwani hatujui tutaokolewa saa ngapi.

Tukiishi kama hawa waliopata ajali hii, hakika hatutadharau yoyote hata kama hajasoma, labda fukara na hatutaona binadamu wengine ni “takataka” – kwani waliooko wengi kwenye ajali hiyo ni watu wa kawaida na wasiokuwa na “kitu.”

Makala haya yamehaririwa kukidhi staili ya Pambazuko.

Majaliwa shujaa, lakini nani awajibike?



Na Dkt. Bullet RUHINDA

NATOA salaam za pole kwa ndugu zetu wote walioondokewa na wapendwa wao kufuatia ajali ya ndege ya Shirika la Precision Air. Watanzania wenzetu na hata watu wa mataifa mengine, waliopoteza maisha Novemba 6, mwaka huu, tuwaombe pumziko la amani.

Katikati ya simanzi ya ajali hiyo, tumempata shujaa; kijana mdogo, Jackson Majaliwa Samwel, aliyevaa ujasiri ambao - bila huo, maisha ya binadamu wenzetu 24 huenda yangepotea pia.

Tuna kila sababu ya kumpongeza kijana huyu. Vijana wa leo wanauliza “tumjengee sanamu wapi?”

Wakati bado jamii bado inajadili kuhusu wapi ajengewe sanamu, Rais Samia Suluhu Hassan akaleta jibu la haraka. Kwamba sasa Majaliwa apatiwe ajira ya kudumu katika jeshi letu la uokozi - Zimamoto.

Kila mtu aliyeguswa na jitihada hizo, angefanya lolote kumpongeza Majaliwa. Tunamshukuru Rais Samia kwa kufanya kitu kikubwa kwa niaba ya nchi.

Pamoja na kumtaka Majaliwa heri, inavyoonekana tumeacha kufanya jambo la msingi kabisa na badala yake watu wengi wamesombwa na upepo wa ushujaa wa kijana huyo kutoka Bukoba, Kagera.

Tumeacha kabisa kujadili uwajibikaji kwa vyombo husika katika ajali hii.

Hatujiulizi mchango wa chombo chetu cha uokozi kama ulifanyika kwa uzito stahili. Je, waokozi – wenye majukumu yao na kulipwa kwa kazi hiyo, walifika kwa wakati, je kama walifika kwa wakati walifanya nini? Je, walikuwa na vifaa gani vya kukabiliana na ajali hii?

Kama hayo yote hayakufanyika kwa kiwango stahiki, mbona hatusikii lolote kutoka kwao? Je, ujuzi wao ulishia pale walipomshuhudia Majaliwa, pamoja na wenzake wakifungua mlango wa ndege na kuwaokoa abiria hao?

Je, watu hawa wenye kazi yao hawakuweza kuokoa hata mtu mwingine mmoja? Watanzania tusikumbwe na kimbunga cha Majaliwa pekee na tukakosa kuhoji mambo ya msingi tunayoyalipia kwa kodi zetu!

Tukiwaacha hao wahusika ambao tunaielezwa kwamba hawakuweza kusaidia sana, tujiulize pia, je, vyombo vyetu vikubwa vya habari vilifanya wajibu wao ipasavyo? Tujiulize, kama vyombo vidogo binafsi viliweza kuhabarisha dunia haraka, vikubwa vilikuwa wapi?

Bado tuna safari ndefu, endapo hatutafanya mabadiliko makubwa ya mfumo na hata utendaji wetu.

Kwa vyombo vikubwa vya habari kushindwa kutoa taarifa sahihi na kwa muda mfupi, sahihi - wananchi walinyimwa fursa na haki ya kupata kile kilichokuwa kikiendelea na badala yake kutegemea wale wanaoitwa “waandishi jamii” ambao hata hivyo walisaidia.

‘Kelele’ za wabunge ni afya

Na Tryruckia MFINANGA

HOJA za wabunge zinazoibuliwa kwa hisia kali katika mijadala, zinachangia kwa kiasi kikubwa serikali kuamua namna nzuri ya kuwatumikia wananchi.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa aliweka wazi mtazamo huo wakati akiahirisha mkutano wa tisa wa Bunge la 12 jijini Dodoma Ijumaa iliyopita. Bunge hilo limeahirishwa hadi Januari 31, 2023.

Baadhi ya wabunge walisikika wakichangia hoja kwa kuzungumza kwa sauti zenye hisia za ukali wakati Bunge lilipokuwa likijadili utendaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu nchini.

Kiongozi huyo wa shughuli za serikali bungeni aliwashukuru wabunge kwa kuibua hoja zenye lengo la kuboresha utendaji wa pamoja na mfumo mzima wa ugharamiaji, upangaji, utoaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu nchini.

“Nyote mtakubaliana nami kwamba lengo la mjadala huo, lilikuwa ni kutafuta suluhu ya suala la wanafunzi takribani 28,000 wenye uhitaji wa kupata mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka 2022/2023 ambao walikuwa hawajapangiwa mikopo, kutokana na ukomo wa kibajeti,” alisema.

Waziri mkuu alibainisha kwamba tayari Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia wanafunzi wote wenye sifa na waliokuwa wamedahiliwa tayari, kuendelea na masomo wakati masuala ya mikopo yao yakifanyiwa kazi.

Akizungumzia utendaji kazi na uwajibikaji wa watumishi wa umma, waziri mkuu alisema serikali imeendelea kuboresha, kuimarisha na kuweka mifumo imara ya usimamizi wa rasilimaliwatu na utendaji kazi wa watumishi wote wa umma ili waweze kuwatumikia vyema wananchi.

Alisema hivi sasa serikali imeweza kuunganisha mifumo ambayo itarahisisha zaidi namna ya kufuatilia utendaji na



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa

maslahi ya kila mtumishi wa serikali.

Waziri mkuu pia alitaja mifumo mingine iliyojengwa kwa lengo la kukabiliana na changamoto za upimaji wa utendaji kazi wa watumishi na mikataba ya utendaji kazi wa taasisi kuwa ni Mfumo wa Kusimamia Utendaji Kazi wa Watumishi wa Umma (PEPMIS) na Mfumo wa Kusimamia Utendaji Kazi wa Taasisi za Umma (PIPMIS).

“Ujenzi wa mifumo hiyo mipya umekamilika. Hivi sasa inafanyiwa majaribio na inatarajiwa kuanza baada ya kukamilika kwa majaribio na kutoa mafunzo kwa watumishi katika taasisi zote za umma,” aliongeza.

Waziri mkuu alisema hatua ya mifumo hiyo kuwa ya kielektroniki itaondoa muhali, hisia za kupendeleana au kuoneana katika usimamizi wa utendaji kazi na itahamasisha uwajibikaji wa hiari wa watumishi wa umma itakayosaidia utoaji huduma bora na kwa wakati kwa umma wa Watanzania.

PSSSF yalamba faida bilioni 582/-

Na Scovya MANASE

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) umeweka rekodi ya kupata faida kubwa inayofikia Sh. bilioni 582 kutokana na uwekezaji.

Pamoja na kupata faida hiyo kubwa, thamani ya mfuko huo imeongezeka na kufikia Sh. trilioni 7.72 hadi kufikia Septemba 30 mwaka huu. Miaka mitano iliyopita, mfuko ulikuwa na thamani ya Sh. trilioni 5.86.

Mkurugenzi mkuu wa mfuko huo, Hosea Kashimba wiki iliyopita jijini Dodoma aliwaeleza waandishi wa habari kwamba PSSSF inajivunia kuwa mfuko ambao umekuwa ukiendelea kupata faida kila mwaka kutokana na uwekezaji wake.

Alitaja maeneo ambayo mfuko huo umewezeza kuwa ni pamoja na uwekezaji katika hatifungani za serikali, majengo ya biashara, uwekezaji wa viwanda, hisa katika kampuni, amana za mabenki na mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

Kashimba alisema kuwa mfuko huu unamiliki majengo ya kupangisha katika miji mbalimbali na kwamba PSSSF imewezeza zaidi ya Sh. bilioni 500 katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

“Hadi kufikia Juni, 2022, mfuko ulikuwa umewezeza kiasi cha shilingi bilioni 130 katika miradi ya viwanda, ambayo iko katika hatua mbalimbali za utekezaji,” aliongeza.

Kutokana na uwekezaji huu, mfuko huo hupata faida ya uwekezaji wa wastani wa asilimia nane kwa mwaka. Kwa mwaka wa fedha ulioisha Juni 2022, PSSF ilipata faida ya uwekezaji, kiasi cha shilingi bilioni 581.72.

Akizungumzia malipo ya pensheni kwa wastaafu, Kashimba alisema wakati wa kuunganishwa kwa mifuko – mwaka 2018, kiasi kilichokuwa kinalipwa ikiwa ni pensheni kwa mwezi kwa wastaafu kilikuwa Sh. bilioni 34, lakini, mpaka kufikia sasa, wastani wa kiasi cha Sh. bilioni 60 kinalipwa bila kukosa kwa



Mkurugenzi mkuu wa PSSF, Hosea Kashimba

wastaafu zaidi ya 150,000 kila ifikapo tarehe 25 ya kila mwezi.

Mwaka 2018, serikali ilitunga sheria ya kuunganisha mifuko kadhaa ya pensheni na kuunda mfuko mmoja wa PSSSF. Mifuko iliyounganishwa ni GEPE, LAPF, PPF na PSPF. Mifuko hii iliunganishwa chini ya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, namba 2 ya mwaka 2018.

Madhumuni ya kuunganisha mifuko hiyo ni kuleta uendelevu wa huduma za pensheni kwa kuondoa ushindani usio na tija, kupunguza gharama za uendeshaji na kuwianisha mafao yanayotolewa na mifuko ya pensheni.

Nguzo ya demokrasia - III

Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA

TUMEKUWA tukiangalia nguzo kadhaa za demokrasia ambazo hutakiwa kusimamia mgawanyo wa madaraka. Leo tutaangazia nguzo ya nne ya demokrasia katika mgawanyo huo.

Maana yake hapa ni kwamba uongozi wa taifa umegawanywa katika matawi au mihimili, ambapo kila tawi lina madaraka yake tofauti na mingine; pia una uhuru wake na wajibu wake katika utendaji pasipo kuingilia na kuingiliwa na matawi mengine.

Ndio ule muundo wa serikali utendao kazi kwa njia ya mihimili ya utawala, bunge na mahakama kama inavyosomeka hata katika katiba inayoongoza taifa letu la Tanzania.

Ufafanuzi huu hautakiwi uwe nadharia tu isiyotekelezwa kwa vitendo. Katika utawala wa demokrasia ya kweli, nguzo hii lazima ionekane kwa wazi katika sheria na ionekane kwa wazi kwa uhai wa serikali. Kazi ya nguzo hii ni kulinda taifa ili lisitumbukie katika utawala wa kidikteta na udhalimu.

Imetokea mara nyingine kwamba mhimili mmojawapo umejiinua juu ya ile mingine. Vilevile imetokea mara nyingine mhimili mmoja au miwili imesujudu na kujitweka chini ya mmoja. Hii hujitokeza kwa kawaida pale katiba na sheria vinapotoa nguvu nyingi zaidi kwa mhili mmojawapo na kusababisha udhaifu katika mihimili iliyobaki.

Kwa upande mwingine udhaifu wa dhamira na uelewa wa viongozi wa mihimili mingine husababisha ukosefu wa uwiano wa nguvu kati ya mihimili.

Mara kadhaa hutokea kwamba katika mataifa dhaifu kidemokrasia, mhimili wa utawala umekuwa kama mshale mrefu kuliko mingine katika podo. Mara nyingi hii hutokea kulingana na katiba za nchi kutoa nguvu kubwa kwa yule anayeongoza mhimili na ambaye hutokea kuwa ndiye kiongozi mkuu wa nchi.



Hii inaendana na ukweli kwamba teuzi nyingi za watendaji wakuu na vyombo mbalimbali, vikiwemo vya ulinzi na usalama, hufanywa na mtawala huyo. Kwa hali hiyo, kuna nguvu kubwa inayozunguka utawala kiasi kwamba mihimili mingine hujikuta ni dhaifu.

Tunapoongelewa mgawanyo wa madaraka tunarudi katika suala zima la uzuri, nguvu na uhuru uliomo katika katiba yenyewe ambayo ndio msingi wa miundo na mifumo ya uendeshaji wa nchi.

Ndio sababu pia nilisema awali kwamba ni lazima katiba itoke kwa wananchi ambayo ndio mwongozo wanawapa watawala na kuelekeza jinsi wanavyotaka taifa lao litawaliwe.

Ndani ya katiba ndimo ambamo wananchi wanaonyesha dhamira yao ya demokrasia ambapo hugawa madaraka kwa matawi yote ya serikali kwa kadiri watakwavyo wa wenyewe.

Kwa hali hiyo ni adimu kwa watawala kutoa hoja ya kuwa na katiba inayogawa madaraka sawa kwa mihimili yote.



Ajali Precision Air itufunze

NIANZE makala haya kwa kutoa salamu za rambirambi kwa familia za wenzetu 19 waliopoteza uhai katika ajali ya ndege iliyotumbukia Ziwa Victoria, Jumapili iliyopita – Novemba 6, mwaka huu.

Kadhhalika natoa salamu za pole kwa majeruhi na kuwatakia uponaji wa haraka.

Vilevile, pongezi nyingi kwa wananchi waliojitoa mhanga kufanya uokoaji. Pongezi za kipekee ziende kwa shujaa Majaliwa Jackson anayeelezwa alifanya kazi kubwa ya uokoaji.

Hata hivyo, kuna mambo mawili yanayosikitisha kuhusiana na ajali hiyo. La kwanza ni maajabu kwamba serikali ilitangaza maombolezo ya kitaifa kufuatia kifo cha Malkia Elizabeti wa Pili wa Uingereza, lakini hakukuwa na maombolezo kwa vifo vya Watanzania wenzetu 19 waliofariki kwenye ajali hiyo.

Sitaki kuamini kuwa kifo cha Malkia huyo wa Uingereza kilikuwa na umuhimu kuliko watu wetu waliopoteza maisha huko Bukoba. Na japo maombolezo ya kitaifa yasingerudisha uhai wa marehemu, utamaduni wetu siku zote ni kuwaenzi wenzetu wanaotangulia mbele za haki.

Jambo jingine ni ukweli mchungu kwamba laiti taasisi husika zingetimiza wajibu wake ipasavyo, huenda ingewezezana kuwaokoa abiria wote waliokuwa kwenye ndege hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana baada ya tukio hilo, marubani wa ndege hiyo waliwasiliana na mamlaka husika kuwafahamisha changamoto walizokuwa wakikabiliana nazo wakati ndege hiyo inajandaa kutua Uwanja wa Ndege wa Bukoba, lakini hawakupatiwa msaada stahili.

Kwa vile lawama hazijengi, ni muhimu



kwa serikali kujifunza katika ajali hiyo, kwa kuimarisha utayari wa kukabiliana na majanga.

Katika pitapita zangu mtandaoni nilikutana na video ya mhandisi mmoja, mwenyeji wa Mkoa wa Kagera, ambaye alieleza kuwa aliwasilisha ripoti ya kitafiti kuhusu hatari zinazoukabili uwanja wa ndege wa Bukoba.

Katika maelezo yake, alieleza kuwa pamoja na matatizo mengine, njia ya ndege kutua uwanjani hapo ni fupi huku akitanabaisha vipimo stahili.

Kadhhalika, alieleza kuhusu changamoto inayotokana na uwanja huo wa ndege kupakana na Ziwa Victoria.

Yayumkinika kuamini kuwa ripoti hiyo haikufanyiwa kazi.

Hata hivyo, kwa vile lawama hazijengi, la muhimu kwa serikali na taasisi husika ni kufanyia kazi upungufu wa kimiundombinu katika uwanja huo na viwanja vingine vya ndege, sambamba na kuimarisha utayari katika kukabiliana na majanga.

Mwisho, kama serikali inavyopokea sifa kwa mikono miwili, inapaswa pia kupokea ukosoaji wenye lengo la kujenga (constructive criticism) kuhusu ajali hiyo.

Hasira za Samia kuonekana leo

Na Shaaban LULELA

KIKAO cha dharura cha Baraza la Mawaziri kinachoketi leo asubuhi Ikulu, jijini Dodoma kitadhihiri ukali wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa wasaidizi wake, Pambazuko limepokezwa.

Kuitwa kwa dharura kwa kikao cha baraza hilo, ambalo kawaida hukutana kila Alhamisi na hatua ya kuutangazia umma, kunaelezwa “kubeba” maana nzito na huenda uamuzi wa baadhi ya mambo yakaushangaza umma na kuwashtua mawaziri wenyewe.

Wiki iliyopita, katika Ikulu ya Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Zuhura Yunus, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kwamba Rais Samia ameitisha kikao cha dharura cha mawaziri ili kujadili ajali ya ndege ya Kampuni ya Precision Air, ambayo ilisababisha vifo vya watu 19.

Wakati ajali hiyo inatokea – Novemba 6, mwaka huu karibu na Uwanja wa Ndege wa Bukoba, kwa kutua ndani ya Ziwa Victoria, Rais Samia alikuwa nje ya nchi.

Taarifa ambazo Pambazuko limezipata ni kwamba katika kikao hicho, pamoja na kuelezwa kuwa na ajenda moja tu ya ajali ya ndege, lakini kutakuwepo na ajenda zingine mbili; kujadili ukame, kukatika kwa umeme mara kwa mara na kukosekana kwa maji, hasa katika Jiji la Dar es Salaam.

Pambazuko limeelezwa kuwa Rais Samia amekasirishwa na namna zoezi la uokoaji wa abiria katika ajali hiyo ya ndege ulivyofanyika na kwamba anataka kupata picha kamili kutoka kwa wahusika.

“Hivi wewe uliwahi kusikia wapi inatangazwatangazwa kwamba mawaziri wanakutana – tena kwa dharura na



Rais Samia Suluhu Hassan

hakuna tishio la vita, lazima kuna kitu kizito kitatokea, subiri” amesema ofisa mmoja wa Ikulu.

“Mama ana hasira na baadhi ya watendaji wake, ambao wanashindwa kuchukua uamuzi kwa haraka na kwa umakini, sasa huenda anaenda kukata mzizi wa fitna, tutasikia leo jioni,” ameongeza.

Akikataa kutajwa jina gazetini, ofisa huyo ambaye jana jioni alikuwa Dodoma, alisema kikao hiki cha dharura kimewaweka “matumbo joto” mawaziri wengi ambao alibainisha wameshawasili katika mji huo – makao makuu ya Tanzania.

“Suala la kukosekana kwa maji Dar es Salaam, nalo linamkera sana rais, anashangaa hakuna mipango inayoonekana kwenda kwa kasi kukabili

Hasira za Samia kuonekana leo

Inatoka Uk. 10



Baraza la Mawaziri kikaoni

ukosefu huo na watu bado wanateseka, tega sikio tu, utanisikia jioni,” amesema.

Jiji la Dar es Salaam linakabiliwa na ukosefu wa maji kwa karibu mwezi mmoja sasa na jitihada zinazoelezwa na wizara na idara na mamlaka za maji zinaonekana “kuelemeza” kwani mipango inayotajwa, ni kama ya zimamoto.

Hivi sasa maeneo mengi ya jiji hilo – ikiwamo Mbweni, Bunju na Tegeta kunauzwa maji lita 1,000 kwa Sh. 40,000. Ndoo moja inauzwa Sh. 1,000 kwa maji ya bomba.

Mbali na kero za maji na kukatika kwa umeme, kukwama kwa huduma hizo, kunaelezwa na wachumi kwamba huzidisha umasikini kwa idadi kubwa ya watu kwani ndiyo msingi wa shughuli nyingi za kuongeza uzalishaji na kipato kwa familia.

Ofisa mwingine kutoka Ikulu alisema pamoja na kujadili ajali ya ndege, lakini suala la kukosekana kwa maji Dar es Salaam, kunamkera Rais Samia na ataliongelea na kujadiliwa kwa kina katika baraza hilo.

“Kuna baadhi ya mawaziri ni mizigo, ni kama wamepwaya kwenye nafasi zao, hawa wanapaswa kuondoka hapo na wawekwe watu wengine wenye uwezo, lakini inaonekana mama (Rais Samia) kama ana huruma sana,” ameingiza ofisa huyo ambaye hakupenda kutajwa jina.

Dkt. Lenny Kasoga, mhadhiri wa vyuo vikuu kadhaa ndani ya nje ya Tanzania, ameliambia Pambazuko kwamba upole wa Rais Samia sasa hauna budi kukoma kwani unamkwamisha kuonekana anachapa kazi.

Amesema wanaomwangusha zaidi ni wasaidizi wake, baadhi ya mawaziri kwani wananchi wamewaona hawawezi kazi, zaidi ya kueleza kwamba “wanashinda mitandaoni” kujisifia ama kubishana na wananchi kwa mambo aliyoeleza hayana tija kwa taifa.

“Kuna hili suala la kuwa na mawaziri kwa uwiano wa kanda ama mikoja, hili anapaswa kuliacha kabisa, achukue wenye uwezo, asiangalie ukanda, njia hiyo imepitwa na wakati na haifai kwa mazingira na nyakati za sasa,” ameingiza msomi huyo na mbozizi katika uchumi.

Dkt. Kasoga anasema maendeleo makubwa ya Tanzania yanakwamishwa kwa kiasi kikubwa na ukosefu wa maono, hasa kwa viongozi wengi wa umma ambao kila uamuzi husubiri rais aseme au awape muongozo, jambo ambalo siyo sawa kwani “linafanya mambo mengine yasiende.”

Anaeleza kuwa baadhi ya mawaziri wanashindwa kuchukua uamuzi hata kwa vitu vidogo, wanasubiri Rais Samia asema ndipo nao “hukurupuka” kuja kwa wananchi.

Rais Mwinyi anakwama wapi?

Na Jabir IDRISSE,
Zanzibar

UHAKIKA ni kwamba Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kutekeleza majukumu yake ya kuongoza nchi, anao washauri wengi.

Ni desturi kwa nchi, hasa zinazoongozwa kidemokrasia, washauri kuwepo ili kumsaidia kiongozi wa nchi kufikia uamuzi wa masuala kadhaa.

Kwa hivyo pasiwe na ubishi katika hili - Rais Dk. Mwinyi anao washauri wa kumshauri kwa baadhi ya mambo anayoamua. Wapo wanaomshauri katika masuala ya uchumi, siasa, afya, michezo na wengine mila na utamaduni wa watu.

Kwa mkazo wa kupunguza gharama - ingawa sijaona kama hili la kupunguza gharama ni jambo linalotiliwa mkazo na uongozi wake - yawezekana Dk. Mwinyi ikawa anatumia mtaalamu wa sheria tu peke yake kwa masuala mbalimbali.

Wakati mwingine hutokea suala la uchumi au siasa na utamaduni yasiatazamwe kwa uzito unaostahili na mwanasheria. Yeye akakazia tu kuwa "kwa hili hapana. Sheria inakataa."

Pengine huibuka shida kidogo ikitokea hali kama hiyo ya fikra za kiongozi kuhusu suala fulani zikenda mtizamo tofauti na ule wa mshauri mtaalamu wa sheria. Maana aghalabu washauri huwa wabobezi wa fani hizi.

Sasa kwa sababu ya asili ya hulka ya binadamu, huenda ikatokea tofauti ya fikra ya kiongozi na mtaalam anayemshauri, hapo kunaweza kuzuka mtafaruku kiasi fulani. Lakini angalau inajulikana kuwa mshauri aliyepo ni mwanataaluma fulani mwenye ujuzi nayo. Na hutokea mara nyingi taaluma yake ikawa ni tofauti na aliyonayo kiongozi anayemshauri.

Utaratibu wa mshauri - kazi ya

kitaalam - ni kufanya kazi yake kwa vile anavyoona ndivyo infaa kwa namna taaluma yenyewe ilivyojengwa. Maana hizi taaluma zina mizizi yake - zimejengwa.

Kuikiuka huwa dhambi ya kimaadili. Basi mtaalam atatoa ushauri wake na kukamilisha. Kama utafuatwa au la! Siyo kazi yake. Uzuri itakuwepo kumbukumbu ya alivyoshauri. Itambeba huko mbele mshauri pakitokea tofauti.

Niseme zaidi hapa; wakati namini Rais Mwinyi anao washauri wa kumpa maoni yao anapotaka kuliendea jambo fulani - iwe kumetokea tatizo au katika amani kabisa, - sina hakika kama washauri alionao ni majasiri kiasi cha kutosha.

Kwamba wana uthubutu wa kusema hapana? Kumwambia rais ukweli wanaojua na kuuamini, na hatari inayochungulia kama uamuzi utapitishwa kwa matakwa au shauku tu ya kiongozi, kinyume na anavoshauriwa? Hili hasa ndo jambo lenye shida kwa viongozi wasiojitambua sawasawa kwamba uamuzi wao unapaswa kuangalia kila upande.

Je, Rais Dkt. Mwinyi anao washauri wanaojiamini? Wamwambie hii ni nyeusi au nyeupe kinyume na aonavyo yeye kiongozi? Labda yeye anaona ile ni nyeusi na siyo nyeupe na hii ni zambarau wala siyo buluu.

Kujiamini kunatakiwa kwenye hali kama hizi za kuyaamua mambo yanayohusu maslahi makubwa ya wananchi nchini kwao. Masuala yenye uhusiano wa moja kwa moja nao wananchi tunaambiwa na Katiba ya Zanzibar kuwa ndio wanaotoa mamlaka kwa kiongozi kwaongozo.

Unapofanywa uteuzi wa viongozi hapana shaka rais atakuwa anashauriwa. Kwamba kwenye "hawa watatu" huyu

Rais Mwinyi anakwama wapi?

Inatoka Uk. 12

na huyu ni stahili. Sijui hufanyikaje mie nafikiria tu.

Hebu tuangalie hili la Rais Mwinyi kumteua Dk. Thabit Idarous Faina kuwa Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC).

Je, ameshauriwa kweli au imekuaje? Tuseme uteuzi huo ndio kweli kilele cha akili na maarifa ya washauri wa Rais Mwinyi? Kwamba huyu ndo sahihi leo anaifaa Tume inayotakiwa iaminike? Ndo hivyo?

Dk. Mwinyi huyu anayepita hadi misikitini kila Ijumaa akihimiza adabu na “amani na utulivu” na kuasa viongozi wenzake wasitafute visingizio vya “kutonesha vidonda?” Leo inakuaje anapoteua kama vile ana jambo lake la ajabu?

Mtu aweza kusema hapana, hakuteua na kwamba huenda “wamemchomekea.” Mbona anasema hataki kufukua makaburi? Sina ubavu wa kuingilia mamlaka yake ya uteuzi - kama inavyochagizwa na wahafidhina - ila najiuliza atateuaje mtendaji ambaye ndo mtuhumiwa namba moja wa kuyachimba makaburi kuhusu uchaguzi uliohujumiwa kwa mipango ya makusudi?

Dkt. Faina alikuwa Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi aliyeondolewa baada ya uchaguzi wenyewe wa 2020 kukamilika. Uchaguzi uliolalamikiwa kwa kila namna na kwa ulivyofisidiwa ukazaa chuki iliyoleta damu ya wananchi kadhaa kumwagwa wakiwemo waliouawa kwa risasi za moto.

Huyo Dkt. Faina baada ya uchaguzi na alipoingia Rais Mwinyi akaunda serikali na alimteua Naibu Katibu Mkuu na baadaye akampandisha kuwa Katibu Mkuu. Na sasa ameamua kumrudisha ZEC.

Wakati wa pilikapilika za uchaguzi ule, wapo baadhi ya watu wanadaiwa



Dkt. Hussein Ali Mwinyi

walifariki dunia wakiwa majumbani kwa majeraha ya risasi na hata vipigo waliyoyapata hata kabla ya siku ya kura.

Haya yanajulikana siyo vyema kuyaeleza kwa kina; nahofia “kutonesha vidonda” ambavyo ajabu vinatoneshwa kwa hatua za kiongozi mkuu.

Hivi yupo anayeamini kuwa matokeo ya uchaguzi ule yaliyoleta Baraza la Wawakilishi la Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa zaidi ya asilimia 98 yaliakisi matakwa halisi ya wapigakura wa Unguja na Pemba? Atakuwa shetani mpenda fitna na mumiani.

Ni vyema Rais Mwinyi akaelewa kuwa ana jukumu na yeye ndo kiongozi mkuu. Na hili ndo uhakika kabisa na kamwe siyo mzaha kama alivyopata kulisema na kujinasibu kuwa ana dhamira njema na Zanzibar.

Kama amesahau kidogo, namkumbusha dhamira huoneshwa kwa matendo siyo maneno mazuri peke yake.

Ni vyema sasa Rais Mwinyi akasimamia na kuonekana anasimamia haki kwa makundi yote ndani ya Zanzibar aache kufanya uteuzi na hata uamuzi ambao unaonekana wazi kuwa kuna maslahi ya kundi alipendalo.

Rais Mwinyi anapaswa kudhihirisha hadharani kabla ya mambo kumzidi - atajafedheheka leo na kesho mbele ya “Hakimu wa Mahakimu.”

Tanzania ikabili umasikini kwa maono mapya, rahisi

Na Godwin CHILEWA, Texas

“HALI ya maisha ni ngumu sana” Haya ndiyo maneno yanayotajwa kila siku, na pengine mara nyingi, kuliko maneno mengine yoyote kwa sasa.

Kila mahali utakapokwenda, utasikia watu wakilalamikia ugumu wa maisha. Tena, tofauti na zamani ambapo waliokuwa wakilalamika ni watu wa kipato cha chini tu, siku hizi hata wafanyabiashara wakubwa, watumishi wa serikali, na hata viongozi wenye nyadhifa kubwa - nao wanalalamika.

Hivi karibuni nilizungumza na jamaa yangu, mtumishi wa serikali, nilipomwambia kuwa hali ya maisha ni ngumu mno, yeye alikataa katakata! Akasema huyo aliyekwambia hali ni ngumu kakudanganya.

Nilipomuuliza ana maana gani, aliniambia hali ya maisha siyo ngumu, ni mbaya! Aliongeza kusema kwamba kule kutumia neno 'hali ni ngumu' ni kupunguza uzito wa hali halisi.

Kwa ujumla hali ngumu ya maisha haiikabili Tanzania peke yake, nchi nyingi duniani, ikiwa pamoja na mataifa makubwa kama Marekani, Uingereza na mengine, yanakabiliwa na changamoto hiyo.

Vita kati ya Russia dhidi ya Ukraine vimesababisha kupanda kwa bei ya mafuta ya kuendesha mitambo na bidhaa nyingine, mabadiliko ya tabia-nchi, yamesababisha kupungua kwa uzalishaji wa chakula na bidhaa za biashara. Pia janga la Covid-19, nalo limesababisha matatizo mengine makubwa ya kijamii na uchumi.

Hivyo, kimsingi mtu mwenye akili timamu hawezi kuilaumu serikali ya Tanzania kwa kuwa chanzo cha matatizo yaliyopo, wananchi wanayo



Rais Samia

kila sababu ya kutathimini na kuhoji mipango na hatua zilizochochuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na serikali katika kupambana na majanga ili kuwapa ahueni ya maisha wananchi.

Pengine changamoto kubwa inayoikabili Tanzania pamoja na nchi nyingine nyingi za Afrika ni kutokuwa na mipango thabiti, na ya muda mrefu, inayolenga kujihami kiuchumi nyakati za majanga.

Udhaifu huu umesababisha wananchi kuumia kila gharama za maisha zinapopanda na maradufu pale uchumi wa dunia unapoyumba.

Mbaya zaidi ni kuwa mambo yanapokuwa magumu, serikali hugeuka kuwakamua zaidi wananchi kwa kodi, tozo na ushuru badala ya kuwapa ruzuku ya kuwasaidia kupunguza makali ya ugumu wa maisha.

Zipo dalili kedekede zinazoonesha kuwa serikali ya Tanzania, ingawa

Tanzania ikabili umasikini kwa maono mapya, rahisi

Inatoka Uk. 14

haijajipanga vyema katika kupambana na dharura au majanga ya kidunia, mojawapo ya dalili hizo ni kutokuwepo kwa akiba kubwa ya mafuta yanayoweza kulikusuma taifa japo kwa miaka miwili endapo vita au janga lolote litajitokeza na kuzuia uingizaji wa mafuta nchini.

Wakati nchi zilizoendelea zimejiwelea akiba ya mafuta ya kuwatosha kwa zaidi ya miaka 20, Tanzania imekuwa ikijivunia kuwa na akiba isiyotosha hata miezi mitatu. Hii ni hatari kubwa kwa nchi inayojitambua.

Pengine kubwa kuliko yote, ni udhaifu wa serikali katika kuwekeza kwenye miradi ya uzalishaji, inayoweza kuwasaidia wananchi kuinua kipato chao.

Bado serikali inasuasua kufanya mikakati ya uwekezaji mkubwa katika kilimo cha mbogamboga, matunda, mpunga na mazao mengine ya chakula na biashara japokuwa ardhi yenye rutuba iko bwelele.

Hili pengine linatokana na mtazamo uliopo nchini hivi sasa kuwa serikali kazi yake ni kukusanya kodi tu, na siyo kujihusisha moja kwa moja na shughuli za biashara au kilimo.

Hata hivyo, ukiziangalia kwa makini nchi nyingi zilizoendelea, utaona kuwa maendeleo ya kilimo, biashara na viwanda katika nchi hizo yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na mikakati ya serikali katika kuwawezesha wakulima hao kwa hali na mali.

Kwa mfano, kilimo cha karanga nchini Marekani kilisitawi baada ya kuzuka kwa wadudu waliokuwa wakishambulia maua ya pamba, zao lililokuwa maarufu zaidi nchini humo, sasa ili kuwasaidia wakulima walioathirika, serikali ilihimiza kilimo cha karanga kwa kutoa ruzuku kwa wakulima, kuhimiza usindikaji wa

mafuta ya karanga, na kuhamasisha ulaji wa siagi iliyotengenezwa kwa karanga (peanut butter).

Leo hii karanga ni mojawapo ya mazao 12 maarufu zaidi nchini Marekani, likichangia kiasi cha dola bilioni moja katika pato la Taifa. Siyo hivyo tu, mkate wenye karanga (peanut butter sandwich) kimekuwa mojawapo ya vyakula vinavyoliwa zaidi nchini humo.

Yote haya ni matokeo ya jitihada ya serikali katika kuwasukuma mbele wakulima na wafanya biashara kwa kuwahakikishia masoko ya uhakika.

Kumbe serikali yetu kama ikidhamiria, nayo inaweza kubadilisha mtazamo wa wananchi katika masuala ya uchumi, hususan wakulima na wafanyabiashara.

Hebu jiulize kwa nini serikali haiweki kiwanda cha kusindika vinywaji vitokanavyo na mabibo mikoa ya kusini, au sehemu nyingine kunakolimwa zao hilo?

Kwa nini tunashindwa kuwa wauzaji wakubwa wa maparachichi duniani wakati kule Mbeya matunda hayo yanaoza tu? Kwa nini tunaagiza mafuta ya kula nje wakati alizeti, chikichi, minazi, karanga, maparachichi na ufuta vimejazana nchini?

Kama wenzetu wanaweza kushawishi mamilioni ya watu kula mkate uliopakwa karanga ili wakulima wao wapate soko, sisi tunakwama wapi?

Napenda kusisitiza haja ya viongozi wetu kuwa na maono mapya katika kuliendelea taifa. Ni ukweli usiopingika kuwa serikali ya awamu iliyopo inajitahidi kupambana ili kubadilisha hali ya maisha ya wananchi, hata hivyo mapambano hayo hayawezi kuwa rahisi, wala kutufikisha mbali kama fikra na mtazamo wa walio wengi utabaki kama ulivyo sasa.

Samia ana kibarua kigumu

Na Mwandishi MAALUM

RAIS Samia Suluhu Hassan, anaweza kupoteza umaarufu wake wa kisiasa, ikiwa serikali anayoingoa itashindwa kuchukua hatua madhubuti kukabiliana na tatizo la ukame nchini.

Taarifa kutoka serikalini, Bunge na Chama Cha Mapinduzi (CCM), zinaeleza kuwa ndani ya kipindi cha miaka Sita ya utawala wa mtangulizi wake, Rais John Magufuli, serikali haikuweza kabisa kwenye miradi ya kuzalisha umeme isiyotegemea mvua.

Vyanzo vya taarifa vinasema, ndani ya kipindi cha miaka sita ya Magufuli, serikali iliweka kando mradi wa “uchumi wa gesi,” uliyobuniwa na serikali ya awamu ya nne, chini ya Rais Jakaya Kikwete, jambo ambalo madhara yake, yameanza kuitikisa utawala wa Rais Samia.

Badala yake, Magufuli alitenga takribani Sh. trilioni 6.5, kwa ajili ya kuanzisha mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere, uliyopo Rufiji mkoani Pwani na ambao uhai wake, unategemea mvua.

Mradi huo, maarufu kama Bwawa la Nyerere, uliolamikiwa na wadau kadhaa wa mazingira, unaripotiwa kuwa umefikia asilimia 74 na utategemea kukamilika mwaka 2024, huku ujenzi wake ukifanyika saa 24 ili kuweza kuukamilisha kwa muda unaotajwa.

Kwa mujibu wa habari hizo, mradi wa umeme wa gesi, uliotajwa na baadhi ya wataalamu kuwa ndio mwarobaini wa kukabiliana na uhaba wa umeme nchini, pamoja na umasikini, umebakia kuwa tegemeo pekee la kuaminika kwa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco).

Taarifa zinasema, asilimia 60 ya umeme unaosambazwa na Tanesco nchini unatokana na gesi inayozalishwa SongoSongo, mkoani Lindi na Mnazi Bay, mkoani Mtwara.



Rais Samia Suluhu Hassan

Uzalishaji wa gesi ulianza mwaka 2004 kwa upande wa SongoSongo na 2006 katika eneo la Mnazi Bay, ambapo gesi yenye futi za ujazo trilioni 57.54, iliyogunduliwa; huku nchi kavu ikiwa futi za ujazo trilioni 10.06 na baharini trilioni 47.48.

Rekodi zinaonyesha miradi miwili mikubwa ya umeme wa gesi ya Kinyelezi I, unaotarajiwa kuzalisha megawati 185 kutoka megawati 70 na Kinyelezi II, inayozalisha megawati 131, ilibuniwa wakati wa utawala wa Kikwete.

Mbali na kuuweka kando mradi wa umeme wa gesi, Serikali ya Magufuli, haikuwekeza kwenye vyanzo vingine vya umeme wa uhakika, kama vile umeme wa upepo, jua na jotoardhi, ili kufikia megawati 3000 hadi 5000 zilizotarajiwa.

“Kama Rais Samia, hatachukua hatua

Endelea Uk. 17

Samia ana kibarua kigumu

madhubuti kukabiliana na uhaba huu wa mvua, unaotokana na mabadiliko ya tabia nchi, anaweza kupoteza umaarufu wake. Hii ni kwa sababu, miaka sita ya utawala wa Magufuli, hakuwekeza kwenye miradi ya umeme na maji, ambayo inaweza kukabiliana na ukame,” ameeleza mbinge mmoja wa zamani wa CCM.

Alisema, “yaani, hili zimwi litamtafuna Mama Samia, wakati tunajua kuwa uhusika wake, unatokana tu na kuwapo kwenye Serikali. Ni muhimu akaliangalia hili mapema na kuanza kuchukua hatua. Vinginevyo, huko mitaani wasiofahamu mambo, hawatamuelewa.”

Aliongeza; “tatizo la ukame, linaathiri wanyama na binadamu. Linaleta njaa na linaweza kusababisha watu kunung’unika na kuuchukia utawala uliyopo. Hivyo basi, siyo jambo la kudharauliwa hata kidogo.”

Kwa upande wa makaa ya mawe, pamoja na Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, kuagiza serikali mara kadhaa, kuanza kwa mradi huo wa miaka mingi iliyopita, uliopo Liganga na Mchuchuma, wilayani Ludewa mkoani Njombe, bado umekuwa ‘ukiimbwa’ bila kutekelezwa.

Kwa takribani miaka 10 kabla ya serikali ya awamu ya tano haijanzia madarakani, upatikanaji wa nishati ya umeme katika mfumo wa gridi ya taifa umekuwa ukiathiriwa na uhaba wa mvua kwa kipindi kirefu.

Kwa mfano, mwaka 2006 uzalishaji wa umeme uliathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na uhaba wa mvua katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2003 hadi 2005, ambapo uzalishaji umeme katika vituo vinavyotumia nguvu za maji ulishuka kwa zaidi ya asilimia 60 baada ya kina cha maji katika Bwawa la Mtera kushuka chini ya kina cha mita 690.00 juu ya usawa wa bahari.

Mwaka 2010, uhaba wa mvua za vuli ulisababisha upungufu wa maji kwenye mabwawa ya kuhifadha maji ya kuzalishia umeme, hususan Bwawa la Mtera ambalo lina uwezo wa kutunza maji ya kuzalisha asilimia 51 ya umeme wa maji kwenye mfumo wa gridi ya taifa.

Upungufu wa umeme ulijirudia tena mwaka 2009 (Septemba – Novemba), ambapo takribani megawati 160 zilikosekana kwenye mfumo wa gridi ya taifa kutokana na upungufu wa maji katika mabwawa ya kuhifadha maji ya kuzalishia umeme pamoja na kuharibika kwa mitambo ya Tanesco na Songas.

Kwa upande wa mradi wa Kinyerezi, ambao ulioanishwa kwenye mpango umeme utekelezaji wake ulioanza mwaka 2013, mradi ulikamilika mwaka 2015 kwa kuhusisha wawekezaji binafsi (PPP).

Katika kuthibitisha kuwa umeme wa gesi, ni muhimu, aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, Profesa Sospiter Muhongo, alieleza kuwa angechaguliwa kuwa rais mwaka 2015, angetumia gesi kuinua uchumi.

Alisema, angefufua uchumi wa gesi na kujenga uwezo wa kuwa na watalamu wa ndani, mambo ambayo hayakuzingatiwa na uongozi uliounda serikali.

Kwenye mradi wa umeme wa upepo, katika kijiji kimoja cha Kititimo uliokuwa na lengo la kuzalisha megawati 100, haukutekelezwa na kwamba utafiti unaonyesha kupitia nishati jadidifu, Tanzania inaweza kuzalisha zaidi ya megawati 20,000 za umeme wa upepo.

Kwa upande wa eneo la maji, serikali ya awamu ya tano, ilitekeleza miradi ya maji 1, 423 yenye thamani Sh. trilioni 1.2, katika miji 28 ikiwemo na Wilaya ya Longido, mkoani Arusha.

Akizunguma na wananchi wa Longido, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema upatikanaji wa huduma ya maji

Samia ana kibarua kigumu

safi na salama vijijini umeongezeka kutoka asilimia 47 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 70 mwaka 2020 na kwa mijini kutoka asilimia 74 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 84 mwaka 2020.

Alisema, mbali ya mradi huo mkubwa wa kutoa maji kutoka Mto Simba mkoani Kilimanjaro hadi Longido, serikali imetoa Sh. bilioni 4.5 kwa ajili ya utekezaji wa mradi wa majisafi katika mji wa Namanga, wilayani humo.

Mradi mwingine mkubwa uliyobuniwa na Serikali ya Awamu ya Tano, ni mradi wa Maji na Umwagiliaji wa kutandaza bomba la maji kutoka Shinyanga hadi Tabora, uliogharimu dola za Marekani milioni 268.35.

Hata hivyo, miradi yote iliyobuniwa na kutekelezwa, uendeshaji wake unategemea mvua, jambo ambalo linaiweka Serikali ya Rais Samia katika mazingira magumu, wakati huu ambako mabadiliko ya tabianchi, yakiripotiwa kuathiri ulimwengu.

“Nadhani tungewekeza kwenye miradi ya kuhifadhi maji, kwa kutumia fedha zilizojengwa Bwawa la Nyerere, tungekuwa mbali sana. Kwa maoni yangu, tusingekuwa na shida hata kidogo kwa kuwa miradi yetu ya gesi ingeendelea kutuletea umeme, huku fedha za hilo bwawa zingelekezwa kwenye maeneo mengine,” anaeleza mbunge huyo.

Naye Anthony Komu, mbunge zamani wa Moshi Vijijini (Chadema), ambaye alikuwa Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Mifugo na Maji, alitolea mfano wa kutekelezwa kwa mradi wa Bwawa la Kitundu, mkoani Morogoro.

Alisema: “Lile Bwawa lina uwezo wa kuzalisha megawati 20 za umeme kwenye gridi ya taifa. Ni bwawa ambalo lingetumika pia kuilisha Ruvu, hivyo pale ambako maji yanapungua Ruvu, kutokuwapo mgawo wa maji.”

Komu alisema, serikali ilipaswa kuanzisha vyanzo vya kuhifadhi maji



Anthony Komu,

kwa kujenga mabwawa katika maeneo ambako maji mengi yanapotea. Alisema, kama Serikali ingeona hilo na kulifanyia kazi, basi pengine ukubwa wa tatizo ungepungua.

Mbali na ukame unaosababisha uhaba wa umeme na maji, janga hilo pia limeanza kuongeza gharama za maisha, ambako bidhaa nyingi zimepanda bei na kusababisha tishio la njaa kwa baadhi ya wananchi.

Vilevile, tatizo la ukame, hadi sasa, limesababisha mamia ya mifugo wa majumbani na wanyamapori, kufa kutokana na kukosa maji na marisho.

Taarifa kutoka mikoa ya Arusha na Manyara, zinaeleza kuwa zaidi ya wanyamapori na mifugo 40,000, tayari wamekufa katika maeneo ya Longido na Babati, jambo ambalo litawafanya wananchi wake kuzidi kuwa masikini.

Habari hii imechapwa hapa kutokana na umuhimu wake. Imechukuliwa kutoka gazeti la Raia Mwema.

Hujambo

Kitenzi 'kuwa' kwa wakati uliopita

Na Dkt. Michael Mashauri

KISWAHILI ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi kubwa kila siku duniani. Vyuu vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

Leo mwalimu ataeleza kuhusu kitenzi “kuwa” kwa wakati uliopita (The verb ‘to be’ Past Tense)

Kitenzi cha ‘kuwa’ katika wakati uliopita uyakinifu hutumia -kuwa ambapo nafasi iliyoachwa katika uyakinifu hujazwa na kiambishi cha upatanishi wa kisarufi na kufuatiwa na

kiambishi cha wakati uliopita (-li-).

Katika ukanushi nafasi hiyo hujazwa na kiambishi cha ukanushi. Katika wingi, hasa wa nafsi ya kwanza, kiambishi cha ukanushi hufuatwa na kiambishi cha upatanisho wa kisarufi cha ngeli husika.

(The verb ‘to be’ in past tense affirmative uses -kuwa whereby the slot left in affirmative is filled by subject concord followed by the prefix of past tense (-li-). In negation the slot is filled by the negation prefix. In plural, especially in the first noun class, negation is followed subject concord of the respective noun class) Examples:

Singular	1 st - Mimi nilikuwa mwalimu (I was a teacher) - Mimi sikuwa mwalimu (I was not a teacher)
	2 nd - Wewe ulikuwa mpole (You were polite) - Wewe hukuwa mpole (You were not polite)
	3 rd - Yeye alikuwa mwema (He/she was kind) - Yeye hakuwa mwema (He/she was not kind)
Plural	1 st - Sisi tulikuwa wanafunzi (We were students) - Sisi hatukuwa wanafunzi (We were not students)
	2 nd - Nyinyi mlikuwa wema (You (all) were kind) - Nyinyi hamkuwa wema (You (all) were not kind)
	3 rd - Wao walikuwa wakarimu (They were generous) - Wao hawakuwa wakarimu (They were not generous)
Singular	- Mti ulikuwa mrefu (A tree was tall) - Mti haukuwa mrefu (A tree was not tall)
	-
Plural	- Miti ilikuwa mirefu (Trees were tall) - Miti haikuwa mirefu (Trees were not tall)
Singular	- Tunda lilikuwa kubwa (A fruit is big) - Tunda halikuwa kubwa (The fruit was not big)
Plural	- Matunda yalikuwa makubwa (Fruits were big) - Matunda hayakuwa makubwa (Fruits were not big)

Ruto aunganishwa ‘udikteka’

**Na Mwandishi MAALUM,
Nairobi**

BAADHI ya vyombo vya habari nchini Kenya vimeendelea kubeba hoja iliyoibuka hivi karibuni kwamba Rais William Ruto ameanza kusuka mipango ili aendelee kuwa madarakani kwa miaka 20.

Kuibuka kwa hoja hiyo, kunashadidiwa zaidi na wapinzani wake wakubwa wa kisiasa, wakiongozwa na aliyekuwa mpinzani wake katika kuwania urais wa nchi hiyo, Raila Odinga.

Katiba ya Kenya inatamka wazi kwamba rais wa nchi hiyo ataongoza kwa mihula miwili ya vipindi vya miaka mitano kila mmoja – hivyo kuwa madarakani kwa miaka 10.

Inaelezwa kuwa dalili uongozi wa chama tawala cha sasa, Kenya Kwanza kupanga kubadili katiba ili kumwezesha Rais Ruto kubaki madarakani zilianza mara tu baada ya kuapishwa.

Aliyeanzisha mchakato huo anatajwa kuwa ni Mbunge wa Fafi, Salah Yakub ambaye anadaiwa kusimamia agenda hiyo ambayo inaonekana kuwakera Wakenya wengi.

Inadaiwa kuwa dalili ya kwanza ya Rais Ruto kutamani kubaki madarakani ni hatua yake ya “kushawishi” wabunge 10 huru ili wajiunge na chama chake.

Kwenye uchaguzi mkuu uliofanyika Agosti 9, mwaka huu, jumla ya wabunge 12 walichaguliwa kupitia utaratibu wa wawaniaji huru.

Wabunge hao walitangaza kuunga mkono Kenya Kwanza baada ya kuungana na wabunge wa mreno huo kwenye kikao cha kwanza walichofanya na Rais Ruto mara tu baada ya kuapishwa kwake.

Baadaye, Rais Ruto aliwakaribisha wabunge saba zaidi kutoka chama cha United Democratic Movement (UDM) kinachoongozwa na Seneta Ali Roba (Mandera).

Ijapokuwa chama hicho kilikuwa katika muungano wa Azimio la Umoja, viongozi wake walidai kuwa



Dkt. William Ruto

walishinikizwa kujiunga na mungano huo “shingo upande”.

Ishara ya tatu ni hatua ya Rais Ruto “kuvamia” ngome za kisiasa za kiongozi wa Azimio, Raila Odinga, na “kunyakua” baadhi ya wabunge waliokuwa wakimuunga mkono.

Hilo lilidhihirishwa na hatua ya Mbunge wa Ugenya, David Ochieng kuwaongoza wanasiasa kadhaa kutoka eneo la Nyanza kutangaza “safari mpya” ya kisiasa kwa kumuunga Rais Ruto. Mbunge huyo alichaguliwa kwa tiketi ya chama chake cha Movement for Democracy and Growth (MDG).

Mbali na hayo, wanasiasa wengine kutoka Nyanza, wakiongozwa na aliyekuwa gavana wa Nairobi, Dkt. Evans Kidero, aliyekuwa mwanaji ugavana katika Kaunti ya Siaya, Nicholas Gumbo, pia walitangaza kumuasi Odinga na kuanza kumuunga Dkt. Ruto.

Anasema kwa kuungwa mkono na wabunge wengi, hilo lilitoiwezesha Kenya Kwanza kushinda nafasi za Uspika katika Bunge la Kitaifa na Seneti mtawalia.

Hili ni kupitia kuchaguliwa kwa Moses Wetang’ula na Amason Kingi kama maspika wa Bunge na Seneti mtawalia.

Hata hivyo, washirika wa Rais Ruto wanataja kauli ya mbunge huyo kuwa “maoni yake binafasi” wala hawana mpango kama huo.

TaiifaLeo

Hoja kutetea uwepo wa Mungu

Na Bruno Marcelo

HOJA za kifalsafa zinazotumiwa na wachamungu kwa ajili ya kutetea uwepo wa Mungu ni nyingi, lakini zinaweza kugawanywa kwenye makundi makuu manne; hoja za kimaadili, hoja za kikosmolojia, hoja za kiteliolojia na hoja za kiontolojia. Nafupisha hoja inayowakilisha kila kundi, lakini bila kuzihakiki.

Hoja mojawapo inayoongelea chanzo cha maadili thabiti (hoja ya kimaadili) inatiririka kama ifuatavyo; Kama Mungu asingekuwapo, kusingekuwapo na maadili thabiti duniani; Lakini, maadili thabiti yapo dunaini; Kwa hiyo, Mungu ambaye ni chimbuko la maadili hayo yupo.

Hoja mojawapo inayoongelea chanzo cha ulimwengu wetu (hoja ya kikosmolojia), inatiririka kama ifuatavyo;

Kila kitu, ambacho ni matokeo, kina chanzo chake; dunia ina chanzo chake, Ali Gazal, mwanazuoni wa Uarabani anasema kuwa chanzo hicho kinaweza kuelezwa kuwa ni nguvu kubwa ambayo akili za kawaida haiwezi kukifikiria, hivyo chanzo hicho anakitaja kuwa ni Mungu.

Hoja mojawapo inayoongelea chanzo cha mpangilio unaonekana ulimwenguni (hoja ya kiteliolojia), inatiririka kama ifuatavyo;

Zana zilizobuniwa na binadamu, kama vile saa, ni matokeo ya ubunifu uliofanywa kwa kutumia akili ya binadamu ili zitumike kufanya kazi fulani; mifumo ya dunia, kama vile jicho, inafanana na vifaa vilivyobuniwa na binadamu; matokeo yanayofanana huwa na sababu zinazofanana; kwa hiyo, ubunifu unaonekana kwenye mifumo ya dunia ni matokeo ya ubunifu uliofanywa na kitu chenye akili kama ya binadamu, lakini iliyo kubwa zaidi; kitu hicho huitwa Mungu; na kwa hiyo Mungu yupo. Hii ni hoja ya Mzungu aitwaye William Paley.

Na hoja mojawapo inayoongelea



Mbingu

piramidi la vitu vyote vilivyomo duniani kuanzia mawe, mimea, wanyama hayawani, watu na vitu vinavyofikirika bila kugusika (hoja ya kiontolojia), inatiririka kama ifuatavyo;

Kama dunia kuna vitu visivyozeeka kama vile ukweli, wekundu, ukijani, uhai, utu, urafiki, na upendo (abstract objects), basi, Mungu asiyezeeka na ambaye ni chimbuko la vitu visivyozeeka, yupo.

Kimantiki, chimbuko la vitu visivyozeeka, haliwezi kuwa akili ya binadamu ambayo inaezeka. Badala yake, kuna akili isivyozeeka, na iliyokuwa inavijua vitu visivyozeeka tangu mwanzo, ikaviumba na kuvipa hifadhi.

Akili isivyozeeka, na ambayo ni makazi ya vitu visivyozeeka, lazima iwe ni kitovu cha ukweli kuhusu vitu vyote duniani na hivyo akili inayojua kila kitu. Akili ya aina hiyo, pia itakuwa na uwezo wa kufanya kila kitu.

Kitu chenye sifa hizi, ndicho huitwa Mungu. Kwa hiyo Mungu yupo. Hii ni hoja ya Mtakatifu Agustino wa Afrika na Kaskazini.

Katiba mpya na maslahi ya wote

Na Deusedith KAHANGWA

TANZANIA ni nchi ya kidemokrasia, yenye kufukuzia ndoto ya uhuru, usawa, na umoja unaotokana na uwepo wa malengo ya pamoja katika taifa. Malengo haya huitwa “maslahi ya watu wote.”

Napenda kujadili dhana hii kwa kuzingatia fikra za Profesa Martin Rhonheimer (73). Huyu alizaliwa mwaka 1950, huko Zurich, nchini Uswis. Na ameandika vitabu zaidi ya vitano. Kitabu kimojawapo ni; “The Common Good of Constitutional Democracy,” cha mwaka 2013.

Fikra zake ninazozijadili hapa ziko kwenye kitabu hiki. Hasa, nataka kujibu swali hili - “maslahi ya pamoja katika taifa lenye mapokeo mseto, lakini lenye kuongozwa kwa mujibu wa katiba ya kidemokrasia, ni kitu gani na siyo kitu gani?”

Profesa Rhonheimer anasema kwamba maslahi ya pamoja katika taifa ni jumla ya taasisi za kijamii zinazowawezesha watu, ama kupitia juhudi binafsi au kupitia juhudi za kimakundi, kukua hadi kufikia ukomo wa ustawi stahiki kulingana na matakwa ya hulka ya binadamu.

Hivyo, maslahi ya pamoja katika taifa yanahusisha: bunge thabiti, serikali sikivu na yenye kuwajibika, mfumo imara wa utoaji haki, mazingira safi na salama, mfumo wa kushughulikia majanga, mfumo wa makazi yaliyopangiliwa, fursa za ajira, mfumo wa huduma za elimu, mfumo wa huduma za afya, mfumo wa miundombinu ya usafirishaji, mfumo wa miundombinu ya mawasiliano, mfumo wa miundombinu ya maji, na mifumo mingine kama hiyo.

Kwa maoni yangu, “maslahi ya pamoja” anayoyaongelea Profesa Rhonheimer, ni kinyume cha “maslahi binafsi.” Kwa kutumia lugha ya kiuchumi, tofauti zake zinaweza kufafanuliwa kama ifuatavyo;

Kwa upande mmoja, katika kuvuna “maslahi binafsi,” yaani “private goods,”



Prof. Rhonheimer

kuna ubaguzi na kuna mchuanio miongoni mwa wanufaika. Mfano ni chakula binafsi, mavazi binafsi, malazi binafsi, gari binafsi, na maegesho binafsi ya magari.

Na kwa upande mwingine, katika kuvuna “maslahi ya wote,” hakuna ubaguzi na hakuna mchuanio miongoni mwa wanufaika. Mfano ni matangazo ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), huduma ya ulinzi inayotolewa na majeshi yetu, mwanga wa jua, na hewa tunayovuta.

Hivyo, anachosema Profesa Rhonheimer ni kwamba, taifa la kiliberali lenye kuongozwa na katiba ya kidemokrasia linazo sifa kuu mbili.

Kwanza, mbali na malengo binafsi ya kila raia, kuna seti ya malengo ya pamoja yanayopaswa kuratibiwa na serikali, kwa sababu wananchi wanata hivyo, na katiba inasema hivyo.

Na pili, kuna seti ya taasisi za kijamii, ambazo zinajenga mazingira mwafaka kwa ajili ya kumwezesha kila raia kufukuzia malengo yake binafsi, lakini bila kumkwaza raia mwingine kufukuzia malengo yake pia.

Kazi pekee ya serikali inapaswa kuongeza usawa na kupunguza utofauti katika jamii kwa kukuza na kuhami maslahi ya wote.

Bado kuna anayem dai Aziz Ki?

Na Babu Jongu

KABLA ya mechi ya Jumatano uliyopita, kati ya Club Africain ya Tunisia na Young African (Yanga) ya Tanzania, kiungo mshambuliaji wa miamba hiyo ya Tanzania, Stephane Aziz Ki, alikuwa na deni kwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

Mashabiki wengi wa soka nchini hasa wale wa Yanga, walikuwa wanalalamikia kiwango chake anachokionyesha tofauti na alivyokuwa kabla ya kusajiliwa Yanga.

Lakini baada ya dakika 90 za mchezo wa Jumatano, kuwania kufuzu hatua ya makundi ya michuano ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), jijini Tunis, Tunisia, ukiwauliza wana Yanga wengi wasio na nongwa, watakuambia hawana deni naye.

Kutokana na umuhimu wa ushindi wa mechi hiyo, goli la Aziz la dakika ya 79 ya mchezo, limelipa kila aina ya deni alilokuwa anadaiwa.

Goli la kuipeleka Yanga hatua ya makundi ya michuano inayoshika nafasi ya pili kwa ukubwa kwa ngazi ya vilabu Afrika, limelipa gharama zote za usajili wake.

Kwa goli lile, Aziz amelipa matusi, kejeli na masimango yote aliyoyapata, Rais wa Yanga, Hersi Saidi, kutoka kwa wapinzani wake wa ndani na nje ya Yanga, kwa kumsajili Aziz kwa gharama kubwa.

Injini Hersi alimsajili Stephane Aziz Ki na mastaa wengine wa kimataifa kwa lengo la kuisaidia Yanga kwenye michuano ya kimataifa.

Kama kuna mwana Yanga aliyekosa usingizi baada ya kutolewa kwenye michuano ya Klabu Bingwa Afrika na Al Hilal ya Sudan, basi usingizi wake umelipwa na Stephane Aziz Ki.

Kama siku Yanga ilipofurushwa na Al Hilal nje ya michuano ya klabu bingwa Afrika, kuna mwana Yanga aliyeshindwa 'kutekeleza majukumu yake ya nyumbani,' iwe kwa mkewe au mumewe, basi Aziz amelipa kwa goli la hilo la usiku



wa Jumatano.

Ushindi wa Yanga dhidi ya Club Africain, umefuta machozi ya kila mshabiki wa Yanga na kuondoa nongwa dhidi ya Aziz mwenyewe na hata kocha wake, Nasrideen Mohammed Naby, aliyekuwa anasimangwa kutofanya vizuri katika michuano ya kimataifa.

Aziz amethibitisha kuwa ni mchezaji mkubwa anayeweza kuamua mechi kubwa.

Aziz ndiye aliamua mechi ya watani; Yanga na Simba kwa kuisawazishia Yanga na kuufanya mchezo kumalizika kwa sare ya 1-1. Na sasa ameamua mechi nyingine kubwa na kuipeleka Yanga hatua ya makundi ya kombe la Shirikisho Barani Afrika.

Kwa ushindi wa Yanga, Aziz atakuwa amelipa deni Yanga na sasa kilichobaki ni kuongeza faida, ambayo nina hakika atawapa.

RC MSTAAFU AKATAA UFUKARA



Msemo wa Wahenga kwamba “mkitaka mali mtazipata shambani” umemjaa mno aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ali Hapi ambaye ameamua kilimo kuwa njia yake ya kusaka chakula menzani, siyo kwake tu, bali na wateja wa mazao ya shambani kwake nje kidogo ya Mji wa Iringa. Hapa anavuna pilipili hoho za njano ambazo zina bei kubwa sokoni. Moja huuzwa hadi Sh. 500. (Picha kutoka ukurasa wake wa Twitter).

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

